Headmaster: +255 689 627 374
Second Master: +255 773 757 199
Email: algebraislamicseminary1@gmail.com
Website: www.algebraschools.ac.tz
algebra islamic seminary

ALGEBRA ISLAMIC SEMINARY
P.O.BOX 36262
SHANGWE - KIGAMBONI
DAR ES SALAAM
TANZANIA - EAST AFRICA

# ALGEBRA ISLAMIC SEMINARY

## JOINING INSTRUCTIONS 2026.

## (MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE)

***REGISTRATION NUMBER: S.4297.***

**FORM ONE 2026.**

**CONTACTS**

**HEAD MASTER**
**PHONE: 0689627374**
**0773757199**

**SCHOOL**
**PHONE: 0715018089**
**0754018089**
**0786280141**
**0616068060**

***This form costs Tsh. 20,000/-***

## UTANGULIZI KUHUSU SHULE:

**ALGEBRA ISLAMIC SEMINARY** ni shule ya **BWENI na KUTWA** ya Kiislamu inayo tazama elimu kuwa ni jambo la kwanza muhimu. Tuna jifunza katika Qur'an kuwa Nabii Adam (A.S) kabla hajaletwa hapa duniani kwa kazi yake ya Ukhalifa alielimishwa kwanza kuhusu mazingira yake (rejea Qur'an 2:31), vile vile tunajifunza kuwa Mtume wa mwisho, Muhammad (s.a.w.) kabla hajaanza kazi yake kubwa ya kuuhuisha Uislamu, alipewa kwanza amri ya kusoma (rejea Qur'an 96:1-5).

Mtume (.S.A.W) amesisitiza kuwa ni faradhi kwa kila Muislamu kutafuta elimu. Tunalojifunza kutoka kwenye Qur'an na Hadithi sahihi za Mtume (s.a.w.) nikuwa:

**Kwanza,** Elimu ni zana ya msingi ambayo Muislamu hana budi kuwa nayo ili aweze kuishi maisha ya Kiislamu na awe Khalifa wa Allaah (s.w.) hapa duniani. **Pili**, tunajifunza kuwa katika Uislamu hapana ubaguzi wa Elimu ya Dini na Elimu ya Dunia. Kila fani ya elimu inayo mwezesha mwanadamu kufikia lengo la kuletwa kwake hapa duniani kuwa Khalifa wa Allaah (s.w) ni faradhi kwa Waislamu.

### LENGO LA SHULE:

Lengo kuu la ALGEBRA ISLAMIC SEMINARY ni kuwaelimisha vijana wa Kiislamu katika maadili ya Kiislamu ili kuwaandaa kuwa viongozi wa kutegemewa na jamii ya Kiislamu na Taifa kwa ujumla kwa kuwakuza kimwili, kiroho na kiakili. Ili kufikia lengo hili shule hii ina lenga kutoa mafunzo katika kiwango cha Kawaida ('O' level) na Kiwango cha Juu ('A' level).

### KAULI MBIU (MOTTO), DHIMA NA DIRA YA SHULE:

- **KAULI MBIU YETU NI**: ***'ELIMU NA MALEZI'***
- **DIRA**: Kuwa shule yenye kuaminiwa Tanzania katika kutoa elimu bora inayoambatana na maadili mema.
- **DHIMA**: Kuwaelimisha wanafunzi kwa gharama nafuu na kuwaongoza katika njia iliyo sahihi kwa kutumia zana za kisasa, walimu mahiri na wenye ari.

### MISINGI NA MAADILI YA SHULE (CORE VALUES):

1. UTAALAMU
2. UBORA
3. HESHIMA
4. HAKI
5. UFANISI
6. UMAHIRI
7. USHIRIKIANO

Masomo yanayofundishwa kwa O'level ni haya yafuatayo:

(i) Elimu ya Dini ya Kiislamu
(ii) Lugha ya Kiarabu
(iii) Qur'an: Kusoma, kuhifadhi, Tafsiri na Mafunzo (Ujumbe)
(iv) Basic Mathematics
(v) Kiswahili
(vi) English language
(vii) Chemistry
(viii) Biology
(ix) Physics
(x) Geography
(xi) History
(xii) Civics
(xiii) Literature in English.
(xiv) Business studies
(xv) Historia ya Tanzania na Maadili.
(xvi) Fasihi ya Kiswahili.
(xvii) UshonI (Garment)
(xviii) Computer science
(xix) Lugha ya Kichina

## NAMNA YA KUFIKA SHULENI

ALGEBRA ISLAMIC SEMINARY ipo katika Wilaya ya Kigamboni kata ya Kibada Jijini Dar es Salaam. Umbali kutoka Ferry kuelekea shuleni ni kilometa kumi na mbili (12km), kutokea Mbagala Kongowe ni kilometa kumi na tano (15km) na kupitia darajani ni kilometa tano (5km). Pakushukia ni kituo cha FULL SHANGWE kama utatumia usafiri wa umma. Geti la shule linatizamana na kituo cha mafuta cha Camel Oil.

## USAFIRI

Wanafunzi watajitegemea kwa usafiri wa kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo. Wasichana wasindikizwe na maharimu wao kama baba, kaka, mjomba, n.k. (Wale ambao wameorodheshwa na kuwekewa picha katika fomu ya kujiunga na shule.

## ADA NA MICHANGO YA SHULE

**Ada ya shule kwa mwaka 2026 ni Tsh 1950,000/ KUTWA NA Tsh 2,950,000/= Kwa wanafunzi wa bweni.**

## MICHANGO

| | | | |
|---|---|---|---|
| BWENI | WASICHANA | Sare za darasani pea 2, sare za kushindia pea 2, mitihani, Bima ya Afya (NHIF), Kitambulisho na Dharura. | **370,000/=** |
| BWENI | WAVULANA | Sare za darasani pea 2, sare za kushindia pea 2, mitihani, Bima ya Afya (NHIF), Kitambulisho na Dharura. | **340,000/=** |
| KUTWA | WASICHANA | Sare za darasani pea 2, sare za kushindia pea 1, mitihani, Bima ya Afya (NHIF), Kitambulisho na Dharura. | **340,000/=** |
| KUTWA | WAVULANA | Sare za darasani pea 2, sare za kushindia pea 1, mitihani, Bima ya Afya (NHIF), Kitambulisho na Dharura. | **320,000/=** |

**NB; Michango yote inalipwa taslimu(cash) katika ofisi ya muhasibu wa shule.**

**Chagua moja kati ya awamu zifuatazo katika kulipa ada ya mwanao:**

**ADA NA MICHANGO YA WANAFUNZI WA KUTWA (WASICHANA)**

| AINA YA MALIPO | MALIPO KWA AWAMU MOJA | MALIPO KWA AWAMU MBILI | | MALIPO KWA AWAMU TATU | | | MALIPO KWA AWAMU NNE | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 30/12/2025 | 30/12/2025 | 30/06/2026 | 30/12/2025 | 30/03/2026 | 30/06/2026 | 30/12/2025 | 30/03/2026 | 30/06/2026 | 30/08/2026 |
| ADA | 1,950,000. | 1,1000,000. | 850,000. | 800,000. | 600,000. | 550,000. | 700,000. | 500,000. | 450,000. | 300,000. |
| MICHANGO | 340,000. | 340,000. | - | 340,000. | - | - | 340,000. | - | - | - |
| **JUMLA** | **2,290,000.** | **1,440,000.** | **850,000.** | **1,140,000.** | **600,000.** | **550,000.** | **1,040,000.** | **500,000.** | **450,000.** | **300,000.** |

**ADA NA MICHANGO YA WANAFUNZI WA KUTWA (WAVULANA)**

| AINA YA MALIPO | MALIPO KWA AWAMU MOJA | MALIPO KWA AWAMU MBILI | | MALIPO KWA AWAMU TATU | | | MALIPO KWA AWAMU NNE | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 30/12/2025 | 30/12/2025 | 30/06/2026 | 30/12/2025 | 30/03/2026 | 30/06/2026 | 30/12/2025 | 30/03/2026 | 30/06/2026 | 30/8/2026 |
| ADA | 1,950,000. | 1,1000,000. | 850,000. | 800,000. | 600,000. | 550,000. | 700,000. | 500,000. | 450,000. | 300,000. |
| MICHANGO | 320,000. | 320,000. | - | 320,000. | - | - | 320,000. | - | - | - |
| **JUMLA** | **2,270,000.** | **1,420,000.** | **850,000.** | **1,120,000.** | **600,000.** | **550,000.** | **1,020,000.** | **500,000.** | **450,000.** | **300,000.** |

## ADA NA MICHANGO YA WANAFUNZI WA BWENI (WASICHANA)

| AINA YA MALIPO | MALIPO KWA AWAMU MOJA | MALIPO KWA AWAMU MBILI | | MALIPO KWA AWAMU TATU | | | MALIPO KWA AWAMU NNE | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 30/12/2025 | 30/12/2025 | 30/06/2026 | 30/12/2025 | 30/03/2026 | 30/06/2026 | 30/12/2025 | 30/03/2026 | 30/06/2026 | 30/08/2026 |
| ADA | 2,950,000. | 1,600,000. | 1,350,000. | 1300,000. | 1000,000. | 650,000. | 1,000,000. | 800,000. | 800,000. | 350,000. |
| MICHANGO | 370,000. | 370,000. | - | 370,000. | - | - | 370,000. | - | - | - |
| **JUMLA** | **3,320,000.** | **1,970,000.** | **1,350,000.** | **1,670,000.** | **1000,000.** | **650,000.** | **1,370,000.** | **800,000.** | **800,000.** | **350,000.** |

## ADA NA MICHANGO YA WANAFUNZI WA BWENI (WAVULANA)

| AINA YA MALIPO | MALIPO KWA AWAMU MOJA | MALIPO KWA AWAMU MBILI | | MALIPO KWA AWAMU TATU | | | MALIPO KWA AWAMU NNE | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 30/12/2025 | 30/12/2025 | 30/06/2026 | 30/12/2025 | 30/03/2026 | 30/06/2026 | 30/12/2025 | 30/03/2026 | 30/06/2026 | 30/08/2026 |
| ADA | 2,950,000. | 1,600,000. | 1,350,000. | 1300,000. | 1000,000. | 650,000. | 1000,000. | 800,000. | 800,000. | 350,000. |
| MICHANGO | 340,000. | 340,000. | - | 340,000. | - | - | 340,000. | - | - | - |
| **JUMLA** | **3290,000.** | **1,940,000.** | **1,350,000.** | **1,640,000.** | **1000,000.** | **650,000.** | **1,340,000.** | **800,000.** | **800,000.** | **350,000.** |

Malipo yote ya fedha za Ada zilipwe Benk katika akaunti za Shule zifuatazo.

CRDB, ACC. NO. **01J1022935000**. AU

AMANA Benk, ACC. NO**. 003120400820001**.

Jina la Akaunti zote ni **ALGEBRA ISLAMIC SEMINARY**

## UTARATIBU WA KULIPA ADA:

Ada yote ilipwe katika Akaunti za Shule, isipokuwa pesa za michango ya shule, ambazo zitalipwa (taslimu) kwa muhasibu wa shule. **Shule haitawajibika na matatizo yoyote yatakayo tokana na ada itakayolipwa mkononi mwa mtumishi yeyote pindi itakapotokea madhara.**

Pay –in-slip iandikwe/ziandikwe jina la mwanafunzi anayelipiwa ada na kidato anachosoma. Mtoto au mzazi awasilishe nakala halisi ya Pay-in-slip kwa Muhasibu wa Shule ili kupatiwa Stakabadhi (risiti) ya malipo.

**NB. Pesa ikishalipwa haitarejeshwa kwa namna yoyote ile.**

- **Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya program maalumu za kitaaluma.**

| S/N | KIFAA | Mwezi January | BEI YA SHULE |
|---|---|---|---|
| 1 | RIM PAPER A4 (Paper line)) | 1 | 20,000/= |
| 2 | RULED PAPER | 1 | 10,000/= |
| 3 | GRAPH PAPER | 1 | 3000/= |
| 4 | SPRING FILE | 1 | 2000/= |
| 5 | BOX FILE | 1 | 5000/= |
| | JUMLA | | 40,000/= |

## 2. MAANDALIZI, MAHITAJI NA VIFAA VYA KUJA NAVYO SHULENI

Ndugu Mzazi/Mlezi, unatakiwa kumuandalia mtoto wako vifaa na mahitaji yafuatayo:

### VIFAA BINAFSI VYA MWANAFUNZI

Kila mwanafunzi atalazimika kuja na vifaa vifuatavyo siku ya kuripoti shuleni. (Pia baadhi vinapatikana shuleni kwa bei iliyoainishwa hapo chini)

| S/N | KIFAA | KIASI | S/N | KIFAA | KIASI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Madaftari 15, (Quire 3 counter book) | 50,000/= | 13 | Soksi nyeupe wasichana na nyeusi wavulana jozi tano. | 5000/= |
| 2 | Mathematical set 1 | 3000/= | 14 | Kiwi na brashi kwa ajili ya kung'arisha viatu. | |
| 3 | Pen box 1 | 8000/= | 15 | Taulo | |
| 4 | Ruler 1 | 1000/= | 16 | Raba za mazoezi | |
| 5 | Godoro futi $2^1/2$ x 4 x 6 | 50,000/= | 17 | Viatu vyeusi vya ngozi vya Kamba na viwe vinavyo funika miguu | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | visiwe na kisigino kirefu wala muundo wa buti | |
| 6 | Shuka 2 pink wasichana na Bluu mpauko kwa wavulana | 20,000/= | 18 | Begi dogo la kubebea madaftari darasani | |
| 7 | Neti (Chandarua) | 12,000/= | 19 | Kanzu na kofia nyeupe (wavulana) | |
| 8 | Tranker la bati (begi la nguo haliruhusiwi.) | 35,000/= | 20 | Sahani ya bati ya vyumba, kikombe na kijiko | 10,000/= |
| 9 | Trak suti (Nyeusi wavulana light blue wasichana) | 26,000/= | 21 | Viatu vya wazi vya kuogea / kutawadhia | |
| 10 | Mashafu (Qur'an) ya Tafsiri (Shekhe Abdullah Saleh Al-farsy) | | | | |
| 11 | Saa ya mkononi ya Alam | | 22 | Ndoo 2 na kopo la kuogea | 10,000/= |
| | Kufuli 2 za Tranker | 6000/= | 23 | Dawa ya meno, mswaki, mafuta ya kujipaka, sabuni ya kufulia na kuogea. | |
| 12 | Nguo za ndani jozi 7 | | 24 | Sweta rangi ya Choklate | 18,000 |
| | | | | | |

**Tanbihi(Muhimu):**

(i) Vitu ambavyo gharama zake hazijaorodheshwa vitanunuliwa nyumbani, mwanafunzi atakujanavyo au utawasiliana na Mkuu wa Shule kwa msaada zaidi kupitia nambari 0689627374/0773757199.

(ii) Ni marufuku mwanafunzi kuvaa mapambo ya aina yoyote wakiwa shuleni au nje ya shule

Perfume, spray zozote haziruhusiwi kwa wanafunzi wote isipokuwa deodorant.

## 6. UANDIKISHWAJI

Siku ya kuripoti Shuleni, Mwanafunzi awe na vifaa vifuatavyo;

(i) Nakala halisi za **Pay-in-slip** ya malipo ya ada na gharama nyingine zote.

(ii) Fomu za utambulisho wa mwanafunzi na wazazi/Mlezi wa mwanafunzi zikiwa zimejazwa na kubandikwa picha.

(iii) Fomu ya daktari (**Medical Examination form**) iliyojazwa na Daktari wa Hospitali ya

Serikali. Kama Mwanafunzi ana matatizo maalum ya kiafya pamoja na tahadhari za kuchukuliwa yaoneshwe kwenye fomu hiyo

(iv) Fomu ya wajibu wa mzazi/mlezi iliyojazwa na mzazi husika
(v) Saa ya Mkononi yenye ALARM.
(vi) Nakala-kivuli cha cheti cha kuzaliwa (photocopy).
(vii) Na vifaa vyote vilivyoorozeshwa katika fomu hiyi.

**MUHIMU:**

1. Fomu zikamilike kwa kubandika picha husika.
2. Uandikishwaji ufanyike katika ofisi ya mkuu wa shule.

## 7. MAENDELEO YA DARASANI

Shule inaweka mkazo mkubwa wanafunzi kusoma kwa bidii ili kuweza kufanya vizuri katika mitihani yao na kuwawezesha kufikia malengo yao, malengo ya wazazi, malengo ya Shule na malengo ya Taifa kwa ujumla. Kwa hiyo shule imeweka utaratibu mzuri wa kuwashindanisha wanafunzi. Hivyo ili mwanafunzi aendelee na kidato kinacho fuata anatakiwa kufikia kiwango cha ufaulu wa daraja la kwanza hadi la tatu (Division I, II au III) na katika somo la Hesabu apate walau ufaulu wa alama D. Mwanafunzi yeyote atakaepata ufaulu wa daraja la nne na zero (Division VI, au O) au katika somo la Hesabu hakupata walau ufaulu wa alama D, katika matokeo ya mwisho wa muhula (muhula I na II) atalazimika kubakia Shuleni kwa wiki mbili kwa ajili ya masomo ya ziada na ufuatiliaji wa karibu zaidi kipindi cha likizo. Na mzazi atalazimika kuchangia gharama ya Tsh 100,000/= kwa ajili ya chakula na huduma nyengine muhimu. **Pamoja na kiwango hicho cha ufaulu nidhamu yake lazima iwe yenye kuridhisha.**

### Kufanya mitihani na kufaulu:

Kila mwanafunzi anapaswa kufanya mitihani yote inayotolewa shuleni. Mwanafunzi asiyefanya mtihani hana budi kutoa taarifa kwa Mwalimu wake wa Darasa ili kama sababu iliyomzuia kufanya mtihani huo niyamsingi apewe mtihani mwingine mara tu dharura iliyomzuia kufanya mtihani itakapokuwa imekwisha

Ikiwa atathibitika kuwa mwanafunzi aliacha kufanya mtihani kwa makusudi au kwa kutoa sababu ambazo hazina mashiko atapewa adhabu kali sana kwa mujibu wa sharia, kanuni na taratibu za Shule yetu, Pia mzazi atachangia kiasi cha Tsh 150,000/= kwa ajili ya gharama za kutunga na kusahihisha mtihani mwengine atakao pewa.

## Udanganyifu katika mitihani:

Kila mwanafunzi analazimika kujiandaa kikamilifu kwa ajili ya mitihani yake. Kitendo chochote cha kufanya au kujaribu kufanya udanganyifu katika mitihani kitahesabika kuwa ni kosa **KUBWA.** Kila atakayebainika **kufanya udanganyifu, mtihani huo utafutwa, atapewa adhabu ya bakora mbele ya wenzake (*assembly)*, Mzazi/Mlezi wake atafahamishwa ili kulipia gharama ya Tsh 200,000/= kwa ajili ya kutunga na kusahihisha mtihani mwingine.** Kama mwanafunzi atarudia kosa la udanganyifu katika mtihani **anaweza kufukuzwa Shule.**

## Kuhifadhi Qur'an

Shule imeimarisha utaratibu wake wa kutathmini uwezo wa wanafunzi katika kusoma na kuhifadhi Qur'an wakati wa kuingia. Kumbukumbu za kila mtoto zitatunzwa na kila mmoja atasaidiwa kulingana na uwezo wake wa kuanzia. Ripoti za kila muhula zitaonesha maendeleo ya mtoto katika kusoma na kuhifadhi. Lengo la shule ni kuwa **mwanafunzi ambaye ameingia shuleni akiwa hajui chochote** katika kusoma na kuhifadhi Qur'an aweze kuhifadhi Juzuu moja kwa kila mwaka (kila kidato), pia mwanafunzi atakae soma kidato cha kwanza hadi cha nne awe na uwezo wa kusoma kwa kuangalia sura zote katiaka msahafu. Wanafunzi watakaozembea watachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kuzuiliwa kuingia darasa linalo fuata.

## Lugha ya mawasiliano:

Lugha rasmi za mawasiliano katika Shule hii ni **KIINGEREZA, KIARABU** na lugha ya KICHINA. Aidha wakati wowote ambao wanafunzi wa Algebra Islamic Seminary watakutana nje ya Shule nilazima waongee lugha hizo tatu rasmi. Shule itaweka mikakati mbalimbali ya kuwezesha hilo kutekelezeka. Wanafunzi wasio jibiidisha katika kujijengea uwezo wa kuwasiliana kwa lugha hizi watachukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu ikiwepo kurudishwa nyumbani au kufukuzwa shule moja kwa moja.

## Vifaa visivyo takiwa (haviruhusiwi)

(i) Kumiliki simu au "line" ya simu, flash, memorycard,
(ii) Kumiliki Radio
(iii) Kumiliki camera/CD za music, mikanda ya aina yoyote.
(iv) Kupaka "perfume" kali kwa (mabinti) navipodozi vya aina yoyote
v. Nguo zenye maandishi, namba au picha na nguo zisizoruhusiwa
vi. Saa yenye radio, simu, remote aump3. (Smart watch)
vii. Nguo za nyumbani

**NB: Vitu hivi akikamatwa navyo mwanafunzi atachukuliwa hatua kali za kinidhamu na havitarudishwa tena (Vitateketezwa).**

## Nidhamu:

- Shule hii ni Seminary ya Kiislamu, hivyo mwenendo wa wafanyakazi na wanafunzi wake unatarajiwa uwe wa Kiislamu. Kukiuka maadili ya Qur'an na Sunnah ni kukiuka maadili ya Shule. Mwanafunzi yeyote atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa atakiuka kwa makusudi maadili ya Qur'an na Sunnah.

## Kazi za nje ya darasa:

- Kufanya bidii katika kazi ni katika nidhamu ya Kiislamu, pia ni katika kutekeleza kauli mbiu ya Shule "ELIMU NA MALEZI" hivyo kila mwanafunzi atawajibika kushiriki kikamilifu katika kazi za usafi wa mazingira, na kazi nyingine kama atakavyo elekezwa na walimu au viongozi wa wanafunzi. Kutegea au kugomea kazi iwe ya darasani au nje ya darasa ni kukiuka maadili anayotakiwa awenayo mwanafunzi wa shule hii, na tabia hii haitovumilika.

### KUWATEMBELEA WANAFUNZI.

- Shule imeweka utaratibu maalumu wa kuwatembelea wanafunzi wa bweni wakati watakapokuwa Shuleni, hiyi ni siku maalumu ambayo wazazi wote watapewa taarifa rasmi kutoka ofisi ya mkuu wa Shule. Pia watakao ruhusiwa kumtembelea mwanafunzi ni wale tu walio orodheeshwa katika fomu ya kujiunga na shule na kuwekewa picha zao.

## 13. KANUNI NA MWENENDO BORA WASHULE

(i) Kila mwanfunzi wa shule hii anapaswa kutambua kuwa yupo hapa kwa ajili ya Uislamu. Kwa sababu hiyo mwenendo wake wa matendo na maneno udhihirishe tabia njema ya Kiislamu.

(ii) Kila mwanafunzi ajitahidi kukuza pendo lake kwa Allah (s.w) na Mtume wake Muhammad (s.a.w) na waislamu wenzake.

(iii) Pamoja nahaki za Muumba zilizo juu ya kila Muislamu, ya mwajibikia kila mwanafunzi achunge haki za nafsi yake na atumie vipaji vyake katika uchamungu ndani na nje ya shule.

(iv) Kila mwanafunzi atumie muda wake vizuri katika kujielimisha kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah (SW).

(v) Kila mwanafunzi atalazimika kuhudhuria Kila kipindi cha somo, kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yote itakayotolewa shuleni. Mwanafunzi atakayeshindwa kuhudhuria darasani kwa siku tatu bila sababu yoyote ya msingi, atakuwa amejifukuzisha shule.

(vi) Wakati wote wa shule au wakati wa kwenda na kurudi likizo vazi rasmi ni sare ya shule. Kutokuwa na sare katika wakati huo ni kosa kisheria.

(vii) Wanafunzi wote wanatakiwa wazingatie kanuni na sheria za mavazi ya Kiislamu wakiwa ndani na nje ya shule. Wasichana wavae nguo za kuenea mwili mzima isipokuwa uso na vitanga vya mikono rejea (24:31). Wavulana wavae nguo za heshima. Nguo kama Khanga, Kaptura, au bukta na nguo nyingine za kihuni haziruhusiwi.

(viii) Ni marufuku kwa mwanafunzi mvulana au msichana kuvaa mapambo aina yoyote.

(ix) Ni marufuku kwa wavulana kuvaa suruali mlegezo, "modal" au carwash, nguo za kubana, n.k

(x) Ni marufuku kwa mwanafunzi mvulana au msichana kuvaa nguo za kubana zinazo onesha rangi ya ngozi ya mwili (Transparent) akiwa shuleni au nje ya shule.

(xi) Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kufuga kucha, kujipaka rangi za kucha, rangi za midomo, kupaka hina, kunyoa nyusi, kuvaa viatu vya kuchuchumia au vinavyotoa sauti, kukali nywele, kutiarangi, kusuka rasta au kubadilisha nywele, kucha, au ngozi kwa namna yeyote ile.

(xii) Ni marufuku mwanafunzi kuchochea, kushawishi, kuhamasisha, au kushiriki mgomo kwa namna moja au nyingine hata kama kuna sababu za msingi. Ni kosa kubwa kugomea amri au maelekezo ya viongozi wa shule kwa ujumla.

(xiii) Wanafunzi wasionekane katika vilabu vya pombe, nyumba za kupangisha wageni (guest house), vibanda vya video au pahala pengine.

(xiv) Kila mwanafunzi ni mlinzi wa mali ya shule, mali zke binafsi na mali za wenzake. Mwanafunzi atakayeharibu, kusababisha mali ya shule kuharibika, kuibiwa au kupotea atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kulipa. Hivyo mwanafunzi atakapogundua wizi wa mali ya shule au ya mwanafunzi mwingine atoe taarifa kwa walimu au viongozi wanaohusika maramoja.

(xv) Kuiba ni kosa kubwa. Mwanafunzi atakayethibitika kuiba ndani ya shule au nje ya shule atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

(xvi) Mwanafunzi anapokuwa na shida yoyote hapa shuleni, kwanza aanze kwa viongozi wa wanafunzi na ndipo aende kumuona mwalimu wa zamu au wa darasa lake, au walimu wengine wanao husika. Kama wanafunzi baada ya kufuata ngazi hizo shida yake haijatatuliwa aende kwa makamu Mkuu wa shule, kisha kwa mkuu wa shule itakapobidi kufanya hivyo mwanafunzi asishitakie shida zake nje ya shule kabla hajamuona mkuu wa shule.

(xvii) Kila mwanafunzi awe msafi na ashiriki vyema katika usafi wa mwili wake binafsi; kitanda, nguo, nywele, kucha, na usafi wa madarasa, bweni, bwalo la chakula na mazingira ya shule kwa jumla.

(xviii) Kelele za aina yoyote hazirusiwi, iwe darasani, kwenye baraza za madarasa, ndani ya bweni, au popote iwe kwa mwanfunzi mmoja mmoja, wengi (kundi). Tunalazimika kuonesha maadili ya Kiislamu katika mazungumzo yetu yote (Rejea Qur`an 31:19).

(xix) Hairusiwi mwanafunzi kulala nje ya eneo la shule bila ya kibali malumu cha maandishi kilicho idhinishwa kutoka kwa mkuu wa shule.

(xx) Mwanafunzi hatakiwi kulala au kwenda katika nyumba za watumishi isipokuwa kwa kibali maalum.

(xxi) Michanganyiko ya wavulana na wasichana hairusiwi. Pale itakapokuwa lazima wanfunzi kuwa pamoja lazima mipaka ya Kiislamu izingatiwe pawe na uangalizi maalum wa walimu.

(xxii) Kupigana ni kosa kubwa. Mwanafunzi atakaye pigana au kumpiga mwenzake atachukuliwa hatua za kinidhamu.

(xxiii) Mwanafunzi anapaswa kuripoti shuleni katika tarehe na muda ulio pangwa. Ikitokea kuchelewa kwa dharura, mzazi au mlezi atoe taarifa kwa uongozi wa shule kabla ya kufunguliwa shule.

(xxiv) Wazazi au walezi watakao watembelea watoto wao shuleni watawajibika kufuata utaratibu ulio wekwa ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na mwalimu wa zamu au mwalimu wa darasa mwalimu wa bweni kabla ya kumuona mtoto. Ifahamike kuwa shule haitahusika kumpatia mzazi/mlezi chakula au malazi atakapomtembelea mwanae.

(xxv) Wakati wa kuwatembelea wanafunzi, mzazi /mlezi harusiwi kuleta vyakula au vinywaji vya aina yoyote kwa wanafunzi, vifaa vitakavyo letwa viwe vile tu vilivyo ruhusiwa na ni vyema vithibitishwe na mwalimu mwenye jukumu hilo kabla ya kukabidhiwa kwa mwanafunzi vikaguliwe.

(xxvi) Wanafunzi hawarusiwi kufanya biashara ya aina yoyote wakiwa shuleni. Kwa hiyo nimarufuku mwanafunzi kuuza vifaa vyake au kununua vifaa vya mwenzake kwa muda wote atakapokuwa shuleni hata ikiwa amemaliza masomo yake. Mwanafunzi anaruhusiwa kutoa sadaka kumpa mwenzake vifaa kama anayoziada.

(xxvii) Zaidi ya mashine ya kufanyia hesabu (calculator), vifaa vya electronics kama vile simu, camera, radio cassette, compyuta, Tv n.k havirusiwi mwanafunzi kuwa navyo katika mazingira ya shule. Mwanafunzi atakaekutwa navyo vitu hivyo hapa shuleni, atachukuliwa hatua kali za kinidhamu.

(xxviii) Nimarufuku kwa wavulana kuwa na nywele ndefu, kukata panki, kiduku, kukata nywele kubwa na ndogo kwa wakati mmoja. Hivyo mwanafunzi wa kiume antakiwa akate nywele ndogondgo kama zinaota muda wote atakapokuwa shuleni na nje ya shule.

(xxix) Wanafunzi wa kike wanaruhusiwa kusuka nywele mtindo mmoja tu wa minyoosho (minyoosho mitano hadi saba) saba au ndindo wa twende kilioni.

(xxx) Kwa wanafunzi wa kutwa watalazimika kusaini wakati wa kuingia na wakati wa kutoka shuleni katika daftari maalumu lililopo getini kwa walinzi.

## MAKOSA YANAYOSABABISHA KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA

Pamoja na maelezo yote hayo, mwanafunzi anaweza kusababisha kufukuzwa shule **mara moja** kama atachupa kwa makusudi mipaka ya Uislamu ikiwa ni pamoja na kanuni za Shule, kufanya makosa ya jinai:

i. Kutosimamisha swala
ii. Wizi wa aina yoyote ile
iii. Kutumia ulevi wa aina yoyote.
iv. Kwenda kwenye dansi au disko au kuandaa/kushiriki katika sherehe yoyote bila idhini ya waalimu/wazazi.
v. Zinaa, kukaribia zinaa kwa namna yoyote ile au kujihusisha na ushoga au usagaji.
vi. Utoro (kutoroka shule kwasababu yoyote ile).
vii. Kuharibu Kwa makusudi Mali yashule/umma.
viii. Kuongoza au kushawishi au kuchochea au kujihusisha katika mgomo wa aina yoyote shuleni au nje ya shule.
ix. Kukataa adhabu halali kwa makusudi.
x. Kuvuruga amani au kuhatarisha amani ya shule au jamii.
xi. Kumomonyoa au kusababisha kumomonyoka kwa maadili ya shule.
xii. Kukiuka kwa makusudi kanuni na taratibu za shule.
xiii. Kutokufanya mitihani au mazoezi ya darasani bila sababu.
xiv. Udanganyifu katika mitihani
xv. Kukosa masomo kwa wiki moja mfululizo.
xvi. Kumiliki simu au chochote kinacho husiana na simu, redion.k.
xvii. Kutukanana au Kupigana au kumpiga mwengine.
xviii. Kufanya mawasiliano yasiyo halali na watu walio nje ya shule
xix. Kuritadi (kutoka katika Uislamu).
xx. Kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi.
xxi. Kufanya mawasiliano nje ya shule kwa kutumia simu ya mtu mwengine nje ya simu ya shule au mwalimu wa darasa.

**HITIMISHO.**

Shule inaendeshwa kwa ushirikiano wa karibu baina ya wafanyakazi wote wa shule, wazazi pamoja na wanafunzi. Hivyo kutakuwa na vikao vya wazazi na uongozi wa shule ili kutoa ushauri kuhusu malezi na taaluma za watoto wetu. hivyo wazazi / walezi watakuwa wakiarifiwa siku za vikao. Natumia fursa hii kwa niaba ya waalimu na wafanyakazi wote wa shule hii kukukaribisha hapa shuleni na naamini utatumia vizuri nafasi hii uliyoipata ya kuongezea elimu yako.

**Mkuu wa shule**
**0689627374 / 0773757199.**

## ORODHA YA VITABU KIDATO CHA KWANZA 2026

| S/N | TITLE | PUBLISHER/AUTHOR |
|---|---|---|
| 1 | History for Secondary Schools | TIE |
| 2 | Kiswahili Shule za Sekondari | TIE |
| 3 | English for Secondary school | TIE |
| 4 | Geography For Secondary Schools | TIE |
| 5 | Historia ya Tanzania na maadili | TIE |
| 6 | Basic Mathematics (Revised Edition) | TIE |
| 7 | Biology | TIE |
| 8 | Physics | TIE |
| 9 | Busssines studies | TIE |
| 10 | chemistry | TIE |
| 11 | Elimu ya Dini ya Kiislamu | TIE |
| 12 | Student Dictionery | Oxford |
| 13 | Mabala the farmer | Ben & company |
| 14 | Hawa the Bus driver | Ben & company |
| 15 | The Magic Garden | |
| 16 | Kalulu the Hare | |
| 17 | Arabic Language | TIE |
| 18 | Qur'an Tafsiri | Shekhe Abdullah Saleh Al-Farsy. |
| | | |

**TANBIHI:**

Kwa mzazi atakayehitaji msaada wa kupatikana vitabu awasiliane na Mkuu wa Shule tu na si vinginevyo kwa nambari **0689627374/0773757199.**